# SHERIA YA MABADILIKO YA NANE KATIKA KATIBA YA NCHI, YA MWAKA 1992

## YALIYOMO


| *Fungu* | *Kichwa cha Habari* |
|---|---|
| 1. | Jina la Sheria na tarehe ya kuanza kutumika. |
| 2. | Matumizi ya Sheria. |
| 3. | Kufanya mabadiliko katika Katiba. |
| 4. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 2(2). |
| 5. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 3. |
| 6. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 9(j). |
| 7. | Kufuta Ibara ya 10. |
| 8. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 13. |
| 9. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 19. |
| 10. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 20. |
| 11. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 32. |
| 12. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 37. |
| 13. | Kufuta na kuweka Ibara ya 39. |
| 14. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 44. |
| 15. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 54. |
| 16. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 59. |
| 17. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 63. |
| 18. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 66. |
| 19. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 67. |
| 20. | Kufuta Ibara ya 69. |
| 21. | Kufuta Ibara ya 70. |
| 22. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 71. |
| 23. | Kufuta na kuweka upya Ibara ya 72. |
| 24. | Kufuta na kuweka upya Ibara ya 74 na 75. |
| 25. | Kufuta na kuweka upya Ibara ya 77 na 78. |
| 26. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 79. |
| 27. | Kufuta Ibara ya 80. |
| 28. | Kufuta na kuweka upya Ibara ya 81. |
| 29. | Kufuta Ibara ya 82. |
| 30. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 83. |
| 31. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 84. |
| 32. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 107. |
| 33. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 129. |
| 34. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 130. |

| *Fungu* | *Kichwa cha Habari* |
|---|---|
| 35. | Kufuta sehemu ya pili ya Sura ya Sita. |
| 36. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 147. |
| 37. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 149. |
| 38. | Kufanya mabadiliko katika Ibara ya 151. |
| 39. | Kufanya mabadiliko katika Nyongeza ya Kwanza. |

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

NO. 4 OF 1992

I ASSENT,

.................................
*President*

29/5/92
.................................

**Sheria ya kufanya mabadiliko katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ili kuondoa mfumo wa chama kimoja cha siasa na kuweka masharti ya kuwezesha mfumo wa vyama vingi vya siasa kufanya kazi**

[ ........................................ ]

IMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jina la Sheria na tarehe ya kuanza kutumika

1.—(1) Sheria hii iitwe Sheria ya Mabadiliko ya Nane Katika Katiba ya Nchi, ya Mwaka 1992.

(2) Sheria hii itaanza kutumika tarehe 1 Julai, 1992.

Matumizi ya Sheria

2 Sheria hii itatumika Tanzania Bara na vilevile Tanzania Zanzibar.

Kufanya mabadiliko katika Katiba

3. Masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya Mwaka 1977 (ambayo katika ibara zifuatazo za Sheria hii itatajwa tu kwa kifupi kama "Katiba"), yanabadilishwa kwa namna ilivyoelezwa katika ibara za Sheria hii zifuatazo.

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 2(2)

4. Ibara ya 2 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko katika ibara ndogo ya (2) kwa kufuta maneno "uliowekwa au kukubaliwa na Chama" na kuweka badala yake "uliowekwa na sheria au kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge".

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 3

**5.** Ibara ya 3 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko—

(a) katika ibara ndogo ya (1), kwa kufuta maneno "yenye chama kimoja cha siasa" na kuweka badala yake maneno "yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa.";

(b) kwa kufuta Ibara ndogo ya (2) na ya (3) na kuweka badala yake ibara ndogo ifuatayo:

"(2) Mambo yote yahusuyo uandikishaji na uendeshaji wa vyama vya siasa nchini yatasimamiwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na ya sheria iliyotungwa na Bunge kwa ajili hiyo.".

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 9(j)

**6.** Ibara ya 9 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko—

(a) kwa kufuta tarakimu "(1)" inayotokea baada ya tarakimu ya ibara ya 9;

(b) katika aya ya (j) ya Ibara hiyo, kwa kufuta maneno "na kwamba Serikali inamiliki njia kuu za uchumi".

Kufuta ibara ya 10

**7.** Ibara ya 10 ya Katiba inafutwa.

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 13

**8.** Ibara ya 13 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko katika ibara ndogo ya (4) —

(a) kwa kuingiza alama ya nukta mara tu baada ya maneno "Mamlaka ya Nchi"; na

(b) kwa kufuta maneno "au ya Chama na vyombo vyake".

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 19

**9.** Ibara ya 19 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko katika ibara ndogo ya (1), kwa kufuta maneno "uchunguzi katika mambo ya dini" na kuweka badala yake "uchaguzi katika mambo ya dini, pamoja na uhuru wa mtu kubadilisha dini au imani yake."

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 20

**10.** Ibara ya 20 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuifuta ibara ndogo ya (2) na kuweka badala yake ibara ndogo zifuatazo:

"(2) Bila ya kujali masharti ya ibara ndogo ya (1), haitakuwa halali kwa chombo chochote cha siasa kuandikishwa ambacho kutokana na Katiba au sera yake —

(a) kinakusudia kukuza au kupigania maslahi ya —

(i) imani au kundi lolote la dini;

(ii) kundi lolote la kikabila pahala watu watokeapo, rangi au jinsia;

(iii) eneo fulani tu katika sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano;

(b) kinapigania kuvunjwa kwa Jamhuri ya Muungano;

(c) kinakubali au kupigania matumizi ya nguvu au mapambano kama njia za kufikia malengo yake ya kisiasa;

(d) kinapigania au kinakusudia kuendesha shughuli zake za kisiasa katika sehemu moja tu ya Jamhuri ya Muungano;

(e) hakiruhusu uongozi wake kuchaguliwa kwa vipindi na kwa njia za kidemokrasia.

(3) Bunge laweza kutunga sheria inayoweka masharti yatakayohakikisha kuwa vyama vya siasa vinazingatia mipaka na vigezo vilivyowekwa na masharti ya ibara ndogo ya (2) kuhusu uhuru na haki ya watu kushirikiana na kujumuika.

(4) Bila ya kuathiri sheria za nchi zinazohusika ni marufuku kwa mtu yeyote kulazimishwa kujiunga na chama chochote au shirika lolote, au kwa chama chochote au cha siasa kukataliwa kusajiliwa kwa sababu tu ya itikadi au falsafa."

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 32

**11.** Ibara ya 32 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko—

(a) kwa kuifuta ibara ndogo ya (3) na kuweka ibara ndogo ya (3) ifuatavyo:

"(3) Endapo inatangazwa kwamba kuna hali ya hatari katika Jamhuri ya Muungano nzima, au katika Tanzania Bara nzima au Tanzania Zanzibar nzima, Rais atatuma mara nakala ya tangazo hilo kwa Spika wa Bunge ambaye, baada ya kushauriana na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, ataitisha mkutano wa Bunge, ndani ya siku zisizozidi kumi na nne, ili kuitafakari hali ya mambo na kuamua kupitisha au kutopitisha azimio, litakaloungwa mkono na kura za wajumbe wasiopungua theluthi mbili ya wajumbe wote, la kuunga mkono tangazo la hali ya hatari lililotolewa na Rais.";

(b) Katika ibara ndogo ya (5)—

(i) kwa kufuta maneno "na Halmashauri Kuu ya Taifa" yanayotokea katika aya ya (c) baada ya neno "Bunge.";

(ii) kwa kufuta maneno "wa pamoja" yanayotokea baada ya neno "mkutano", na pia maneno "na Halmashauri Kuu ya Taifa" yanayotokea baada ya neno "Bunge", katika aya ya (d).

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 37

**12.** Ibara ya 37 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko—

(a) katika ibara ndogo ya (1), kwa kufuta maneno "Mbali na kuzingatia masharti yaliyomo katika Katiba hii, sheria za Jamhuri ya Muungano na siasa na maagizo ya Chama," na kuweka badala yake maneno yafuatayo:

"Mbali na kuzingatia masharti yaliyomo katika Katiba hii na katika sheria za Jamhuri ya Muungano,";

(b) kwa kuifuta ibara ndogo ya (2) na kuweka ibara ndogo ifuatayo:—

"(2) Endapo Baraza la Mawaziri litaona kuwa Rais hawezi kumudu kazi zake kwa sababu ya maradhi ya mwili au ya akili, laweza kuwasilisha kwa Jaji Mkuu azimio la kumwomba Jaji Mkuu athibitishe kwamba Rais, kwa sababu ya maradhi ya mwili au ya akili hawezi kumudu kazi zake. Baada ya kupokea azimio kama hilo, Jaji Mkuu atateua bodi ya utabibu ya watu wasiopungua watatu atakaowateua kutoka miongoni mwa mabingwa wanaotambuliwa na sheria ya matabibu ya Tanzania, na bodi hiyo itachunguza suala hilo na kumshauri Jaji Mkuu ipasavyo, naye aweza, baada ya kutafakari ushahidi wa kitabibu kuwasilisha kwa Spika hati ya kuthibitisha kwamba Rais, kutokana na maradhi ya mwili au ya akili, hamudu kazi zake; na iwapo Jaji Mkuu hatabatilisha tamko hilo ndani ya siku saba kutokana na Rais kupata nafuu na kurejea kazini, basi itahesabiwa kwamba kiti cha Rais kiwazi, na masharti yaliyomo katika ibara ndogo ya (3) yatatumika.".

Kufuta na kuweka ibara ya 39

**13.** Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuifuta ibara ya 39 na kuweka badala yake masharti yafuatayo—

"Sifa za mtu kuchaguliwa kuwa Rais

**39.** Mtu hatastahili kuchaguliwa kushika kiti cha Rais wa Jamhuri ya Muungano isipokuwa tu kama—

(a) ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa Sheria ya Uraia;

(b) ametimiza umri wa miaka arobaini;

(c) ni mwanachama, na mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa;

(d) anazo sifa za kumwezesha kuwa Mbunge au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.".

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 44

**14.** Ibara ya 44 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuifuta ibara ndogo ya (2) ya ibara hiyo na kuweka ibara ndogo mpya ifuatayo:

"(2) Baada ya kutoa tangazo, Rais atapeleka nakala ya tangazo hilo kwa Spika wa Bunge ambaye, baada ya kushauriana na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya tangazo, ataitisha mkutano wa Bunge ili kuitafakari hali ya mambo na kufikiria kupitisha au kutopitisha azimio la kuunga mkono tangazo la vita lililotolewa na Rais."

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 54

**15.** Ibara ya 54 ya Katiba inafanya mabadiliko kwa—

(a) kuweka baada ya ibara ndogo ya (3) ibara ifuatayo:

"(4) Mwanasheria Mkuu wa Serikali atahudhuria mikutano yote ya Baraza la Mawaziri na atakuwa na haki zote za mjumbe wa mikutano hiyo isipokuwa hatakuwa na haki ya kupiga kura katika mikutano hiyo."

(b) kuibadilisha ibara ndogo ya (4) ya sasa iwe ibara ndogo ya (5).

**16.** Ibara ya 59 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuifuta ibara ndogo ya (5) na kuweka badala yake ibara ndogo ifuatayo: Kufanya mabadiliko katika ibara ya 59

"(5) Mwanasheria Mkuu atakuwa Mbunge kutokana na wadhifa wake, atashika madaraka yake mpaka—

(a) uteuzi wake utakapofutwa na rais, au

(b) mara tu kabla ya Rais mteule kushika madaraka ya Rais, na atalipwa mshahara, posho na malipo mengine kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge."

**17.** Ibara ya 63 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko— Kufanya mabadiliko katika ibara ya 63

(a) katika ibara ndogo ya (3)—

(i) kwa kuweka alama ya nukta badala ya nukta-mkato mwishoni mwa aya ya (d), na

(ii) kwa kuifuta aya ya (e); na

(b) kwa kuifuta ibara ndogo ya (4).

**18.** Ibara ya 66 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuifuta ibara ndogo ya (1) ya ibara hiyo na kuweka ibara ndogo mpya ifuatayo: Kufanya mabadiliko katika ibara ya 66

"(1) Bila ya kuathiri masharti mengine ya ibara hii, kutakuwa na aina zifuatazo za Wabunge, yaani—

(a) Wabunge waliochaguliwa kuwakilisha majimbo ya uchaguzi;

(b) Wabunge wanawake ambao watakuwa ni asilimia kumi na tano ya Wabunge waliotajwa katika aya ya (a), (c) na (d), waliochaguliwa na vyama vya siasa vinavyowakilishwa Bungeni, kwa mujibu wa ibara ya 78, na kwa kuzingatia masharti ya uwiano wa uwakilishi baina ya vyama hivyo;

(c) Wabunge watano waliochaguliwa na Baraza la Wawakilishi kutoka miongoni mwa wajumbe wake;

(d) Mwanasheria Mkuu."

**19.** Ibara ya 67 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko— Kufanya mabadiliko katika ibara ya 67

(a) katika ibara ndogo ya (1), kwa kuifuta aya ya (a) na ya (b) na kuweka badala yake aya zifuatazo:

"(a) ni raia wa Jamhuri ya Muungano aliyetimiza umri wa miaka ishirini na moja, na ambaye anajua kusoma na kuandika katika Kiswahili au Kiingereza.

(b) ni mwanachama na ni mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa;";

(c) kwa kuifuta aya ya (c) ya ibara ndogo ya (1);

(i) kufuta aya ya (e),

(ii) kufuta aya ya (g) na kuweka badala yake aya ifuatayo:

"(g) ikiwa mtu huyo ameshika madaraka ya afisa mwandamizi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, isipokuwa madaraka

ambayo Rais aweza au anatakiwa kukabidhi kwa Mbunge kwa mujibu wa Katiba hii au sheria iliyotungwa na Bunge;";

(iii) kufuta aya ya (i), (j), (k), (l) na (m);";

(d) kwa kufuta ibara ndogo ya (9), (10), (11) na ya (12).

Kufuta ibara ya 69

**20.** Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuifuta ibara ya 69.

Kufuta ibara ya 70

**21.** Ibara ya 70 ya Katiba inafutwa.

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 71

**22.** Ibara ya 71 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko—

(a) katika ibara ndogo ya (1)—

(i) kwa kufuta katika aya ya (a) ya ibara ndogo ya (1) fungu la maneno linaloanza na maneno "isipokuwa kwamba" mpaka maneno "Bara au Tanzania Zanzibar" katika aya ya (ii)";

(ii) kwa kufuta aya ya (e) na kuweka badala yake aya ifuatayo:

(ii) "(e) ikiwa Mbunge ataacha kuwa mwanachama wa chama alichokuwamo wakati alipochaguliwa au alipoteuliwa kuwa Mbunge;";

(iii) kwa kufuta aya ya (f).

(b) katika ibara ndogo ya (2) kwa kufuta maneno "au kosa la kutoa habari za uongo kwa kiapo, kinyume cha Sheria ya Kanuni ya Jinai, kuhusu tamko rasmi lililotolewa kwa mujibu wa masharti ya ibara ya 69 ya Katiba hii".

Kufuta na kuweka upya ibara ya 72

**23.** Ibara ya 72 ya Katiba inafutwa na badala yake kutakuwa na ibara mpya ifuatayo:

"Watu wenye madaraka Serikalini kukoma utumishi wanapo-chaguliwa

**72.** Iwapo mtu yeyote mwenye madaraka katika utumishi wa Serikali, madaraka ya aina iliyotajwa katika ibara ya 67(2)(g) ataamua kuwa mgombea uchaguzi wa Rais au wa nafasi nyingine yoyote chini ya Katiba hii, mtu huyo atahesabiwa kuwa utumishi wake umekoma tangu tarehe ya tarehe ytake ya kuwa mgombea uchaguzi.".

Kufuta na kuweka upya ibara ya 74 na 75

**24.** Ibara ya 74 na ya 75 zitafutwa na badala yake kunawekwa ibara mpya zifuatazo:

"Tume ya Uchaguzi

**74.**—(1) Kutakuwa na Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao watakaoteuliwa na Rais:—

(a) Jaji wa Mahakama Kuu au Jaji wa Mahakama ya Rufani, ambaye atakuwa mwenyekiti;

(b) Makamu wa Mwenyekiti;

(c) Wajumbe wengine watakaotajwa na Sheria iliyotungwa na Bunge.

(2) Rais atamteua Makamu wa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi kwa kufuata kanuni kwamba endapo Mwenyekiti ni mtu anayetoka sehemu moja ya Muungano, Makamu wake atakuwa ni mtu anayetoka sehemu ya pili ya Muungano."

(3) Watu wafuatao hawataweza kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume ya Uchaguzi yaani—

(a) Waziri au Naibu Waziri;

(b) mtu mwenye madaraka ya aina yoyote iliyotajwa mahsusi na Sheria iliyotungwa na Bunge kwamba ni mwiko kwa mtu mwenye madaraka hayo kuwa mjumbe wa Tume ya Uchaguzi;

(c) Mbunge au mtu mwingine mwenye madaraka ya aina yaliyotajwa na Sheria iliyotungwa na Bunge kwa mujibu wa masharti ya aya ya (g) ya ibara ndogo ya (2) ya ibara ya 67 ya Katiba hii.

(d) Kiongozi wa chama chochote cha siasa.

(4) Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya ibara hii, Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi atakoma kuwa Mjumbe litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo—

(a) ukimalizika muda wa miaka mitano tangu alipoteuliwa; au

(b) ikiwa litatokea jambo lolote ambalo, kama asingekuwa Mjumbe wa Tume, lingemfanya asiweze kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi.

(5) Rais aweza tu kumwondoa katika madaraka Mjumbe wa Tume ya Uchaguzi kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi zake, ama kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote, au kwa sababu ya tabia mbaya au kupoteza sifa za kuwa mjumbe.

(6) Majukumu ya Tume ya Uchaguzi yatakuwa ni—

(a) kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura katika uchaguzi wa Rais na Wabunge katika Jamhuri ya Muungano;

(b) kusimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi wa Rais na Wabunge; na

(c) kuchunguza mipaka na kuigawa Jamhuri ya Muungano katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya uchaguzi wa Wabunge.

(7) Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu yake, Tume ya Uchaguzi itakuwa ni idara inayojitegemea, na mtendaji mkuu wake atakuwa ni Mkurugenzi wa Uchaguzi ambaye atateuliwa na kufanya kazi kwa mujibu wa masharti ya Sheria iliyotungwa na Bunge.

(8) Bunge laweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti ya kuweka utaratibu wa kusimamia uchaguzi wa Wabunge wanaowakilisha wilaya ya uchaguzi.

(9) Tume ya Uchaguzi yaweza kutekeleza shughuli zake bila ya kujali kwamba kuna nafasi miongoni mwa viti vya Wajumbe au kwamba Mjumbe mmojawapo hayupo, lakini kila uamuzi wa Tume ni lazima uungwe mkono na wajumbe walio wengi kati ya Wajumbe wote wa Tume.

(10) Bunge laweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti ya kuweka utaratibu wa kuwateua Wajumbe wa kusimamia uchaguzi wa Wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi na, bila ya kuathiri masharti ya Sheria kama hiyo au maagizo ya Tume ya Uchaguzi, madaraka ya Tume ya Uchaguzi ya kusimamia uchaguzi yaweza kutekelezwa na Wajumbe hao.

(11) Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, Tume ya Uchaguzi haitalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali, au maoni ya chama chochote cha siasa.

(12) Hakuna mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza jambo lolote lililotendwa na Tume ya Uchaguzi katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

(13) Katika utekelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa Katiba hii, Tume ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano itashauriana mara kwa mara na Tume ya Uchaguzi ya Tanzania Zanzibar.

Majimbo ya uchaguzi

**75.**—(1) Bila ya kuathiri masharti mengineyo yaliyo katika ibara hii, Jamhuri ya Muungano itagawanywa katika majimbo ya uchaguzi kwa idadi na kwa namna itakavyoamuliwa na Tume ya Uchaguzi baada ya kupata kibali cha Rais.

(2) Bila ya kuathiri sheria yoyote inayotumika kuhusu mambo hayo, Tume ya Uchaguzi, baada ya kupata kibali cha Rais itakuwa na mamlaka ya kuweka mipaka ya majimbo ya uchaguzi.

(3) Katika kuweka mipaka ya majimbo ya uchaguzi, Tume ya Uchaguzi itazingatia ipasavyo upatikanaji wa njia za mawasiliano, na pia hali ya kijiografia ya eneo linalokusudiwa kugawanywa katika majimbo ya uchaguzi.

(4) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii na ya Sheria yoyote inayohusika na mgawanyo wa nchi katika majimbo ya uchaguzi, Tume ya Uchaguzi yaweza mara kwa mara, na angalao kila baada ya miaka kumi, kuchunguza mgawanyo wa Jamhuri ya Muungano katika majimbo ya uchaguzi, na yaweza kubadilisha majimbo ya uchaguzi kama matokeo ya uchunguzi huo au kutokana na matokeo ya hesabu ya watu wote katika Jamhuri ya Muungano.

(5) Endapo baada ya uchunguzi kufanywa kuhusu mgawanyo wa Jamhuri ya Muungano katika majimbo ya uchaguzi kunafanyika mabadiliko katika majimbo ya uchaguzi, au katika idadi ya Wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi au mabadiliko kwa idadi ya majimbo ya uchaguzi au idadi ya Wabunge, basi mabadiliko yatakayotokea katika idadi ya Wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi yataanza kutumika wakati Bunge litakapovunjwa tena baada ya kutokea mabadiliko hayo ya idadi ya majimbo au idadi ya Wabunge katika majimbo ya uchaguzi.

(6) Bila ya kujali masharti mengineyo ya ibara hii, hakuna mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza jambo lolote lililotendwa na Tume katika utekelezaji wake wa kugawa Jamhuri ya Muungano katika majimbo ya uchaguzi.".

**25.** Ibara ya 77 na 78 zinafutwa na badala yake kunawekwa ibara mpya zifuatazo: Kufuta na kuweka upya ibara ya 77 na ya 78

"Utaratibu wa uchaguzi wa wabunge wa majimbo ya uchaguzi

77.—(1) Wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi watachaguliwa na wananchi kwa kufuata masharti ya Katiba hii na vilevile masharti ya Sheria iliyotungwa na Bunge kwa mujibu wa Katiba hii inayoweka masharti kuhusu uchaguzi wa Wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi.

(2) Isipokuwa pale ambapo Tume ya Uchaguzi, kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au Sheria iliyotungwa na Bunge kwa ajili hiyo, itaagiza vinginevyo, kutachaguliwa Mbunge mmoja tu katika jimbo la uchaguzi.

(3) Wagombea uchaguzi katika jimbo la uchaguzi watatakiwa watimize masharti yafuatayo—

(a) wawe wamependekezwa mmoja mmoja, na chama cha siasa kinachoshiriki uchaguzi katika jimbo hilo;

(b) wamewasilisha majina yao kwa Tume ya Uchaguzi kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Sheria iliyotungwa na Bunge au uliofafanuliwa na Tume kwa mujibu wa sheria.

Utaratibu wa uchaguzi wa Wabunge wanawake

"78.—(1) Kwa madhumuni ya uchaguzi wa Wabunge Wanawake waliotajwa katika ibara ya 66 (1) (b), vyama vya siasa vilivyoshiriki uchaguzi, kwa kufuata utaratibu uliowekwa, vitapendekeza kwa Tume ya Uchaguzi majina ya wanawake kwa kuzingatia masharti ya uwiano wa uwakilishi baina ya vyama vilivyoshinda uchaguzi katika majimbo na kupata viti Bungeni. Tume ikiridhika kuwa mtu yeyote aliyependekezwa anazo sifa za kuwa Mbunge itamtangaza kuwa amechaguliwa kuwa Mbunge, na masharti ya ibara ya 83 ya Katiba hii yatatumika kuhusu kuchaguliwa kwa mtu huyo kuwa Mbunge."

(2) Mtu yeyote hataweza kupendekezwa na chama chochote cha siasa kwa ajili ya uchaguzi kwa mujibu wa ibara hii ila tu iwapo anazo sifa za kustahili kuchaguliwa zilizotajwa na masharti ya ibara ya 67 ya Katiba hii.

(3) Majina ya watu waliopendekezwa kwa mujibu wa ibara ndogo ya (1) na Tume ya Uchaguzi yatatangazwa kama matokeo ya uchaguzi baada ya Tume kuridhika kwamba masharti ya Katiba na Sheria yanayohusika yamezingatiwa.

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 79

**26.** Ibara ya 79 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kufuta maneno "ibara ya 66(1)(d)" na kuweka badala yake "ibara ya 66 (1)(c)".

Kufuta ibara ya 80

**27.** Ibara ya 80 ya Katiba inafutwa.

Kufuta na kuweka upya ibara ya 81

**28.** Ibara ya 81 ya Katiba inafutwa na badala yake kunawekwa ibara mpya ifuatayo:—

"**81.** Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya Katiba hii, Tume ya Uchaguzi yaweza kuweka masharti yanayofafanua utaratibu utakaotumiwa na vyama vya siasa kwa ajili ya kuchagua na kupendekeza majina ya Wabunge wa aina iliyotajwa katika ibara ya 66 (1) (b)."

Kufuta ibara ya 82

**29.** Ibara ya 82 ya Katiba inafutwa.

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 83

**30.** Ibara ya 83 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko—

(a) kwa kuifuta ibara ndogo ya (1) na kuweka badala yake ibara ndogo ifuatayo—

"(1) Kila shauri kwa ajili ya kupata uamuzi juu ya suala—

(a) kama uchaguzi au uteuzi wa mtu yeyote kuwa Mbunge ulikuwa halali au sivyo; au

(b) kama Mbunge amekoma kuwa Mbunge na kiti chake katika Bunge ki wazi au hapana,

litafunguliwa na kusikilizwa kwanza katika Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (2) ya ibara hii.";

(b) kwa kuifuta ibara ndogo ya (3) ya (4), na kuweka badala yake ibara ndogo zifuatazo:

"(3) Bunge laweza kutunga Sheria kwa ajili ya kuweka masharti kuhusu mambo yafuatayo—

(a) watu wanaoweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu kwa ajili ya kupata uamuzi juu ya suala lolote kwa mujibu wa masharti ya ibara hii;

(b) sababu na nyakati za kufungua shauri la namna hiyo, utaratibu wa kufungua shauri na masharti yanayotakiwa yatimizwe kwa kila shauri kama hilo; na

(c) kutaja mamlaka ya Mahakama Kuu juu ya shauri kama hilo na kueleza utaratibu wa kusikiliza shauri lenyewe.

(4) Kutakuwa na haki ya kukata rufaa mbele ya Mahakama ya Rufani ya Tanzania kupinga uamuzi wa Mahakama Kuu juu ya shauri lolote lililosikilizwa kwa mujibu wa masharti ya ibara hii."

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 84

**31.** Ibara ya 84 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko—

(a) kwa kufuta ibara ndogo ya (3), ya (4), ya (5) na ya (6); na

(b) katika ibara ndogo ya (7), kwa kufuta aya ya (e) ya (f) na ya (g).

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 107

**32.** Ibara ya 107 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kufuta ibara ndogo ya (4) ya ibara hiyo.

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 129

**33.** Ibara ya 129 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko, katika ibara ndogo ya (4), kwa kufuta maneno "Viongozi wa Chama", na kuwekwa badala yake maneno "Viongozi wa vyama vya siasa wanaoshughulikia mambo ya umma,".

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 130

**34.** Ibara ya 130 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko, katika ibara ndogo ya (2), kwa kufuta neno "Chama" na kuweka badala yake maneno "chama chochote cha siasa."

Kufuta sehemu ya pili ya Sura ya Sita

**35.** Kichwa cha habari na masharti yoye ya Sehemu ya Pili ya Sura ya Sita ya Katiba vinafutwa.

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 147

**36.** Ibara ya 147 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuongeza baada ya ibara ndogo ya (2) ibara ndogo zifuatazo:

"(3) Itakuwa ni marufuku kwa mwanajeshi yeyote kujiunga na chama chochote cha siasa, isipokuwa tu kwamba atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika ibara ya 5 ya Katiba hii.

(4) Kwa madhumuni ya ibara hii, mwanajeshi maana yake ni askari aliyeajiriwa kwa masharti ya muda au ya kudumu katika Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza au Jeshi la Kujenga Taifa.".

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 149

**37.** Ibara ya 149 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko katika ibara ndogo ya (1) kwa kufuta aya ya (b) na kuweka badala yake aya mpya ifuatayo:

"(b) iwapo mtu huyo ni Rais, basi taarifa hiyo ya kujiuzulu ataiwasilisha kwa Spika;".

Kufanya mabadiliko katika ibara ya 151

**38.** Ibara ya 151 ya Katiba inafanyiwa mabadiliko—

(a) katika ibara ndogo ya (1), kwa kufuta ufafanuzi wa neno "Chama" na kuweka badala yake ufafanuzi ufuatao:

""Chama cha Siasa" maana yake ni chama cha Siasa kilichoandikishwa kikamilifu kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa, ya Mwaka 1992;".

(b) katika ibara ndogo ya (2), kwa kufuta aya ya (c) na kuweka badala yake aya ifuatayo:

"(c) iwapo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii kuna jambo lolote linalotakiwa litekelezwe au lishughulikiwe na Chama chochote cha siasa, basi, jambo hilo litatekelezwa au litashughulikiwa na chama hicho kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na chama hicho kwa ajili hiyo, na pia kwa kuzingatia masharti ya Katiba hii au Sheria yoyote iliyotungwa na Bunge kwa ajili hiyo;".

Kufanya mabadiliko katika Nyongeza ya Kwanza

**39.** Nyongeza ya Kwanza ya Katiba inafanyiwa mabadiliko kwa kuongeza, baada ya aya ya 21 inayotaja Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano, aya mpya ifuatayo:

"22. Uandikishaji wa Vyama vya Siasa na mambo mengine yanayohusiana navyo."

Passed in the National Assembly on the seventh day of May, 1992.

*Clerk of the National Assembly*

Imepigwachapa na Mpiga Chapa wa Serikali, Dar es Salaam—Tanzania